MATAMASHA YA UTAMADUNI

1.0 Utangulizi:

Tamasha ni utaratibu wa kufanya jambo lenye shughuli nyingi kwa pamoja au zinazofuatana kwa karibu. Shughuli hizo zinaweza kuwa za aina moja au fani moja peke yake, kama vile ngoma, muziki, tamthilia, mashairi, vitabu, sanaa za ufundi au michezo. Aidha tamasha linaweza kuwa la mchanganyiko wa fani mbili au zaidi kwa pamoja. Sifa nyingine muhimu ya tamasha ni kwa shughuli kufanyika katika muda mfupi na mfululizo – saa chache siku chache au wiki chache. Sifa ya tatu muhimu ni kwa shughuli za tamasha kufanyika sehemu moja au sehemu kadhaa zilizo karibu karibu kuwezesha washiriki – watendaji na watazamaji - kutembelea maeneo yote husika katika muda wa tamasha zima. Inasisitizwa kuwa fani zinazoshirikishwa katika tamasha ziwe zenye ubora wa juu na kila inapowezekana baadhi yake zitokane na wabunifu au mapendekezo ya wahakiki na wahifadhi mahiri na maarufu katika jamii au nchi. Aidha utaratibu wa mashindano huweza kuandaliwa katika sehemu na ngazi mbalimbali ili kupata fani bora za kushirikishwa katika tamasha.

2.0 Madhumuni ya Matamasha:

Kwa mujibu wa dhana na mpangilio wa shughuli, tamasha huwa na mvuto wa hali ya juu na kishindo kikubwa katika jamii. Kwa sababu hiyo matamasha yanasaidia sana katika:-

2.1 Utambulisho:

Utambulisho ni kitu muhimu kwa binadamu. Wakati wote binadamu hufanya jitihada ya kujitambua yeye mwenyewe na kubainisha wenzake. Utamaduni ni moja ya nguzo muhimu za utambulisho wa mtu. Matamasha hutoa fursa kwa mtu binafsi na jamii kwa jumla kujua na kukumbuka wao ni nani – kama jamii, kama taifa – na kuendelea kuishi au kufanya mambo kwa kuzingatia jamii au taifa lake. Kwa upande mmoja

mtu hujiona kuwa mwenye fahari, heshima na nguvu. Kwa upande mwingine utambulisho huu huwa chanzo cha kuheshimu na kuzingatia misingi ya jamii au taifa ya maadili, itikadi, mahusiano ya kiuchumi, kisiasa na tabia njema.

2.2 Mshikamano:

Mshikamano katika jamii hutokana na jamii husika kuwa na kitambulisho na dhamira moja. Matamasha huwa ni kielelezo cha utamaduni na huipa jamii ari katika nafsi zao ya kuendelea kuwa na mshikamano, umoja na ushirikiano na maelewano miongoni mwao.

2.3 Usawa na Demokrasia:

Katika nchi nyingi ipo hali ya baadhi ya jamii au vikundi kujihisi wanyonge, kudharauliwa au kudhalilishwa. Katika hali hii usawa baina ya wananchi huwa haupo. Ushiriki wa jamii au vikundi hivi katika tamasha huwajengea heshima na kujiamini mbele ya wenzao na kwa hiyo dhana ya usawa na demokrasia kuimarika.

2.4 Ushindani:

Ushindani ni chachu muhimu ya maendeleo. Washiriki katika tamasha lolote huwa na nia ya kufanya vizuri. Hali hii huamsha vipaji vya wabunifu na watunzi wa fani za utamaduni na kuwezesha maendeleo makubwa ya fani hizo.

2.5 Uzoefu na Elimu

Matamasha ni mahali ambapo vitu vingi huonyeshwa, kuzungumzwa au kutolewa maandishi. Hivi vyote huwa na fursa nzuri kwa watunzi, wabunifu, wanataaluma, wanafunzi na wananchi kwa jumla kupata uzoefu na elimu zaidi katika mambo ya utamaduni.

2.6 Urithishaji:

Tamasha hushirikisha mchanganyiko wa watu wa rika, uzoefu na ujuzi mbalimbali. Aidha watu wazima au wazee hupata fursa ya kushiriki kuonyesha ujuzi wao. Kwa hiyo tamasha huwa ni fursa ya wazee kuweza kurithisha mambo muhimu ya taifa kwa vizazi vipya. Aidha tamasha huhamasisha shughuli za ufufuaji na uendelezaji wa urithi wa utamaduni unaoshikika na usioshikika.

2.7 Ushabiki wa kitaifa:

Kutokana na wingi na uzuri wa mambo/vitu vinavyoonyeshwa katika tamasha, ushabiki na upenzi mkubwa kwa taifa huweza kuibuka miongoni mwa wananchi. Tofauti zao za siasa, maeneo au itikadi huziweka kando.

2.8 Biashara na Uchumi:

Kutokana na mambo au vitu vingi vizuri kuonyeshwa katika tamasha, wadau na wafanya biashara wengi wa kazi za utamaduni huweza kuhudhuria na kubaini mwelekeo wa biashara au shughuli zao. Aidha sehemu ambayo tamasha litafanyika kutakuwa na fursa kubwa ya kupanua biashara kwa bidhaa mbalimbali za sehemu hiyo kama vile vyakula na malazi.

2.9 Burudani:

Binadamu ni kiumbe ambaye huwa na hamu ya kuburudika ikiwa ni njia ya kujenga nguvu na ari zaidi katika kazi. Kwa hiyo matamasha hukidhi hamu ya wananchi ya burudani kwa kiwango cha juu na manufaa makubwa.

3.0 Hali ya Matamasha Nchini:

Katika nyakati mbalimbali, kumepata kuwepo na matamasha na mpaka leo bado kuna matamasha yanayoendelea kuendeshwa.

3.1 Tamasha la Sanaa la Bagamoyo

Chuo cha Sanaa Bagamoyo kilianzisha tamasha hili mwaka 1982 ikiwa ni kioo cha kazi za walimu na wanafunzi wake. Ingawa tangu mwanzo ulikuwepo ushiriki wa watu wa nje ya chuo, ni hivi sasa ndiyo ushiriki huo umepanuka hadi kufikia asilimia 96 ya maonyesho yote kutoka asilimia 15 mwaka 1982. Aidha upo ushiriki wa wasanii kutoka nje ya nchi ambao kila mwaka huwa kati ya asilimia 10 – 15 ya ushiriki wote wa tamasha. Shughuli zinazoendeshwa katika tamasha hilo ni:

(a) Sanaa za jukwaani za ngoma, tamthiliya, muziki na sarakasi.
(b) Sanaa za Ufundi za uchoraji, uchongaji, ufinyanzi, ususi, ufumaji, mavazi.
(c) Warsha za kitaalamu
(d) Makongamano
(e) Maandamano ya wasanii katika mitaa ya Bagamoyo.

Tamasha hili hufanyika kila mwaka, mwishoni mwa mwezi Septemba.

3.2 Tamasha la Utamaduni wa Mzanzibari

Tamasha hili huendeshwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Lengo lake kuu ni kuonyesha fani mbalimbali za Utamaduni wa Wazanzibari. Hata hivyo kuna washiriki ambao hualikwa kutoka Tanzania Bara na nchi za nje. Fani zinazoonyeshwa ni ngoma, muziki, sanaa za ufundi, mavazi na maandamano.

Tamasha hili hufanyika katika mwezi wa Julai kila mwaka na imekuwa jadi kwa Rais wa Zanzibar kulifungua.

3.3 Tamasha la Filamu la Zanzibar (ZIFF)

Tamasha hili huendeshwa na Shirika la Watu binafsi na ni la kimataifa. Hufanyika kila mwaka katika miezi ya Juni na Julai katika Miji ya Zanzibar, Kisiwani Unguja na Chakechake Kisiwani Pemba. Ingawa kimsingi ni tamasha la filamu, huhusisha pia sanaa za jukwaani na za ufundi. Filamu zinazonyeshwa katika tamasha kutoka nchi mbalimbali katika Bara la Afrika na Mabara mengine, hususan Ulaya na Asia. Vikundi vya sanaa za jukwaani kutoka nje ya nchi pia hushiriki. Aidha kuna warsha na makongamano mbalimbali kuhusu maeneo mbalimbali ya fani za filamu na utamaduni kwa jumla.

3.4 Matamasha ya Sanaa za Watoto

Matamasha haya ni sehemu ya mradi wa sanaa kwa watoto ambao unaendeshwa na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa ushirikiano na Wizara ya Elimu na Utamaduni na Baraza la Sanaa la Taifa. Tamasha la kwanza lilifanyika mwaka 1990 na yameendelea kufanyika kila mwaka. Wanaoshiriki katika matamasha haya ni zile shule zilizo katika mradi ambazo ni 60 za Dar es Salaam, 5 za Bagamoyo na 5 za Morogoro. Shule za Bagamoyo na Morogoro hufanya matamasha yao mwezi Juni na za Dar es Salaam hufanya tamasha lao mwezi Septemba. Mambo yaanyoonyeshwa katika matamasha haya ni sanaa za jukwaani, yaani ngoma, muziki, tamthilia, sarakasi na ngonjera. Aidha kuna warsha, maonyesho ya filamu na vitabu.

3.5 Tamasha la TUSEME

TUSEME ni mradi wa sanaa kwa wanafunzi wa shule za Sekondari za wasichana na mchanganyiko. Jumla ya Shule 23 kutoka mikoa 20 ya

Tanzania Bara zinashiriki katika mradi huu. Madhumuni ya mradi ni kutumia sanaa katika kuwawezesha wanafunzi wa kike kuboresha uwezo wao wa taaluma, kuwapa stadi za kupambana na kubezwa na kudhalilishwa kwa wanawake na kuimarisha demokrasia.

Tamasha ambalo ni sehemu ya mradi, Tamasha hufanyika katika mwezi wa Februari au Machi kila mwaka Mjini Dar es Salaam na Shule zote za mradi hushiriki. Tamasha la kwanza lllifanyika mwaka 1997.

3.6 Tamasha la CHASAMATA:

CHASAMATA ni Chama cha Sanaa za Maonyesho Tanzania, ambacho kilianzishwa mwaka 1977. Chama hiki kimekuwa kikififia na kuibuka. Tangu mwaka 1998 kimerudia uhai wake na moja ya shughuli kinazozifanya ni kuandaa na kuendesha matamasha. Tamasha la kwanza lilifanyika mwaka 2001 na la tatu 2003. Matamasha ya chama hiki hujihusisha zaidi na utoaji elimu dhidi ya Ukimwi. Fani zinazoshirikishwa ni sanaa za jukwaani, hususan ngoma na tamthiliya. Washiriki wa tamasha ni vikundi wanachama wao wa Mkoa wa Dar es Salaam tu. Tamasha hufanyika katika wiki ya kwanza na ya pili ya Desemba kila mwaka.

3.7 Tamasha la Ukaguru

Tamasha hili huandaliwa na Shirika lisilo la Serikali Children and Youth Development (CHAYODE) ambalo Makao yake makuu yako katika Mji wa Morogoro. Tamasha hili linahusika na kusherehekea utamaduni wa Jamii ya Wakaguru Wilayani Kilosa na hufanyika Gairo. Tamasha la kwanza lilifanyika mwaka 2000 na lilishirikisha vikundi vya ngoma na muziki asilia vya Jamii ya Wakaguru. CHAYODE ina mpango wa kulipanua tamasha hili ili lihusishe jamii zote za Mkoa wa Morogoro.

3.8 Tamasha la Vitabu

Tamashala hili huandaliwa na wadau wa vitabu ikiwa pamoja na Bodi ya Huduma ya Maktaba Tanzania, PATA, UWAVITA na makampuni ya uchapishaji na uchapaji wa vitabu. Hufanyika katika mwezi wa Septemba kila mwaka.

3.9 Siku ya Kiswahili

Hili ni tamasha la maadhimisho ya matumizi ya Kiswahili. Tamasha huandaliwa na kuendeshwa na Baraza la Kiswahili la Taifa, BAKITA mwezi Februari kila mwaka. Baadhi ya shughuli katika tamasha hili ni maonyesho ya vitabu, fani za lugha kama vile mashairi, makongamano na kutoa tuzo kwa asasi au watu binafsi waliodhihirika kuchangia.

3.10 Wiki ya Mfuko wa Utamaduni Tanzania

Tamasha hili huandaliwa na Mfuko wa Utamaduni Tanzania. Kwa kawaida hufanyika katika wiki ya kwanza ya Novemba. Sasa hivi limehamishiwa wiki ya kwanza ya Desemba kupisha mfungo wa Ramadhani. Shughuli za tamasha huwa pamoja na maonyesho ya kazi zilizofadhiliwa na Mfuko, Uzinduzi wa vitabu au majarida, semina, warsha na kutunuku Tuzo ya Zeze kwa wateule wa mwaka husika.

3.11 Tamasha la Muziki la Busara

Tamasha hili lilianza mwaka huu huko Zanzibar na lengo lake ni kuonyesha muziki wa nchi za Majahazi, ikiwemo taarab.

3.12 Maonyesho ya Sanaa Bora ya Taifa

Maonyesho haya yameanza mwaka huu na yataendelea kuandaliwa, ikiwezekana kila mwaka. Madhumuni yake ni kutoa fursa kwa Wasanii Mahiri kuonyesha na kuuza sanaa zao.

3.13 Matamasha ya nchi za Mashariki ya Afrika

Eastern Africa Theatre Institute ilianzishwa na kuandikishwa nchini Tanzania – Makao Makuu yake – mwaka 1999. Nchi wanachama ni Ethiopia, Kenya, Tanzania na Uganda. Mojaya shughuli zake ni kuandaa matamasha katika nchi wanachama. Tamasha la kwanza lilifanyika Ethiopia mwaka 2000, la pili Uganda mwaka 2002 na la tatu litafanyika Kenya mwaka 2004. Tanzania itakuwa mwenyeji wa tamasha la taasisi hii mwaka 2006. Tamasha hili hushirikisha fani za sanaa za maonyesho, hususan ngoma na tamthilia. Wahusika hutoka katika nchi wanachama.

3.14 Matamasha ya nchi za SADC:

Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika – SADC, imeandaa ratiba ya matamasha kati ya sasa hadi 20/2 kama ifuatavyo.

2004	-	Tamasha la Muziki	-	Zambia
2006	-	Tamasha la fani mchanganyiko		?
2008	-	Tamasha la Tamthiliya	-	Tanzania
2010	-	Tamasha la fani mchanganyiko	-	?
2012	-	Tamasha la Sanaa za Ufundi	-	Malawi

Kama inavyoonyesha, matamasha haya yatafanyika kila baada ya miaka miwili na yatapishana kati ya matamasha ya fani moja na fani mchanganyiko. Tanzania tumeomba kuwa wenyeji wa tamasha la tamthilia la 2008.

3.15 Matamasha ya Mara Mojamoja

Yapo matamasha mengine ambayo si ya kudumu bali hufanyika mara waandaji wanapokuwa na mpango na uwezo wa kuyaendesha bila ya mpango wa kurudia tena. Mengi ya matamasha haya huwa na madhumuni maalumu kama vile uzinduzi wa asasi au shughuli, utangazaji wa bidhaa, sherehe maalumu au mpango wa mauzo, kupata fedha, kutunisha mfuko au kuchangisha fedha kwa shughuli za hisani.

4.0. Mantiki ya Tamasha la Utamaduni la Taifa

Pamoja na kuwepo matamasha mbalimbali kuna mantiki ya kuwepo kwa tamasha la taifa.

4.1. Upeo

Upeo wa matamasha yaliyopo sasa ni mfinyu. Matamasha haya hayafikii ngazi ya taifa zima kwa jiografia au kwa aina ya washiriki. Ngazi ya tamasha la taifa mpaka sasa iko wazi na inahitaji kuzibwa. Ari ya kushiriki ya wana-Utamaduni haikidhiwi kikamilifu kwa kukosekana ngazi hii ambayo wangeweza kuiweka mikakati ya kuifikia katika malengo au ndoto zao. Aidha matamasha madogo yanaweza kuwa mahali pa kuchagulia washiriki wa tamasha la taifa.

4.2. Kiwango cha Ushirikishwaji

Ushiriki katika matamasha yaliyopo sasa ni mdogo kulingana na malengo, madhumuni na mtandao wake kijiografia. Wana–Utamaduni wengi hujikuta hawana sifa ya kushiriki au kushirikisha fani zao katika matamasha haya. Tamasha la Taifa ni la Watanzania wote. Hata kama nafasi za kushiriki haziwezi kuwaenea wote, kila mmoja atakuwa na haki ya kushindania nafazi hizo.

4.3 Anuai

Anuai katika utamaduni husaidia kuonyesha utajiri wa utamaduni na kujenga hali ya kupendeza. Matamasha ya jumla yana uwezo wa kushirikisha aina mbalimbali za fani za utamaduni zenye anuai pana zaidi.

4.4 Mvuto

Ingawa matamasha yote yana asili ya kuwa na mvuto mkubwa kwa washiriki na jamii, tamasha la jumla lina mvuto mkubwa zaidi kwa wana-utamaduni, wadau, mapromota na wafanya biashara wa ndani na nje ya nchi.

5.0. Mchanganuo wa uwezo, udhaifu, fursa na matishio katika kuendedha Tamasha la Taifa

5.1. Uwezo:

(a) Maamuzi ya Kisera

(i) Katika Sura ya Saba ya Sera ya Utamaduni ya 1997 imehimizwa kwa wananchi kushiriki na kushirikishwa katika shughuli za utamaduni kwa kuwa ni haki yao. Hii ina maana kuwa wananchi ni muhimu kuwawezesha kufanya hivyo kwa kuweka mipango na mazingira mazuri.

(ii) Mpango wa Utekelezaji wa Sera ya Utamaduni unayo programu ya kuanzisha na kuendesha matamasha ya aina na ngazi mbalimbali, likiwemo Tamasha la Utamaduni la Taifa.

(b) Katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala, CCM, imeelekezwa kuwa Serikali itaboresha shughuli za maendeleo ya utamaduni, hususani kwa kuanzisha na kusimamia mashindano na matamasha yatakayowashirikisha wananchi wengi katika michezo na sanaa kwa lengo la

kupata wachezaji na wasanii hodari katika ngazi ya taifa na mataifa.

(i) Uwezo wa kupanga, kusimamia na kuendesha matamasha upo.

- Idara za Serikali zote mbili zenye dhima ya kusimamia maeneo mbalimbali ya utamaduni
- Idara za Utamaduni za Wilaya na Miji
- Makumbusho ya Taifa.
- BASATA
- BAKITA
- BASAZA
- BAKIZA
- Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Idara ya Sanaa na Sanaa za Maonyesho
- Chuo cha Sanaa, Bagamoyo
- Mfuko wa Utamaduni Tanzania.

(ii) Asasi zisizo za Serikali na vyama vya hiari zinaweza kushirikishwa katika kazi hii.

- Chama cha Wasanii wachongaji Tanzania (CHAWASAWATA)
- Chama cha Wachoraji Tanzania
- Chama cha Sanaa za Maonyesho Tanzania (CHAMASAMATA)
- Umoja wa Waandishi wa Vitabu Tanzania (UWAVITA).
- Chama cha Usanifu wa Kiswahili na Ushairi Tanzania (UKUTA)
- Tanzania Theatre Centre (TzTC)
- Eastern Africa Theatre Institute (EATI)

- Uzima kwa Sanaa (UZIKWASA)

(c) Utaalamu wa kubaini fani zinazofaa kushirikishwa katika tamasha na wastadi za kuendesha maonyesho upo. Utaalamu huu unapatikana katika asasi za umma za umma, mashirika yasiyo ya Serikali, vyama vya hiari na watu binafsi. Kutokana na jinsi sekta ya Utamaduni inavyofanya kazi kwa ushirikiano, upo urahisi wa kutumia wataalamu hawa katika shughuli za tamasha.

(d) Fani, shughuli, au vitu vya kuonyeshwa katika tamasha hili vipo kwa wingi. Hii inatokana na utajiri mkubwa wa utamaduni wetu. Cha muhimu ni kuwa makini katika uchaguzi ili kuwa na tamasha lenye anuai pana.

5.2. Udhaifu

(a) Ufinyu wa bajeti ya serikali na mashirika ni udhaifu ambao bado upo. Pamoja na kwamba hali inaanza kuwa nzuri, kiasi kinachotengwa kwa ajili ya shughuli za Utamaduni katika Wizara, Mashirika na Halmashauri za Wilaya na Miji na ni kidogo kuweza kubeba mahitaji ya kuendesha shughuli za tamasha. Upo umuhimu wa mgao kwa utamaduni kuongezwa. Aidha ni muhimu kubuni njia nyingine za kupata fedha za ziada. Ni lazima pia kutumia utaratibu ambao utagawa jukumu la ugharimiaji kwa wadau mbalimbali.

(b) Tatizo la upungufu wa watumishi katika ngazi za Mkoa na Wilaya ni kubwa. Kwa mujibu wa mfumo wa Serikali uliopo sasa, hakuna afisa utamaduni katika ngazi ya Mkoa. Kwa kutambua umuhimu wa masuala ya utamaduni, mikoa imekabidhi shughuli za utamaduni ama katika Idara ya Elimu, Idara ya Kazi na Maendeleo ya Jamii kwa kushikiza tu, siyo wajibu kamili . Halmashauri za

Wilaya na Miji zilizo nyingi zinao Maafisautamaduni. Hata hivyo baadhi ya Halmashauri hazina maafisa hawa. Ni muhimu kuzingatia hali hii na kuandaa utaratibu utakaofanikisha tamasha.

(c) Miundombinu kama vile kumbi za maonyesho ya sanaa za jukwaani na za ufundi ni tatizo si tu katika ngazi ya Wilaya bali pia katika Makao Makuu ya Mikoa. Pia sehemu za malazi zinaweza kuwa haba kwa baadhi ya Mikoa. Aidha vifaa muhimu vya maonyesho vya taa za jukwaa na vipaza sauti vina shida ya kupatikana katika baadhi ya Mikoa. Kwa hali hii ni lazima kuchagua Mikoa yenye nafuu kuwa wenyeji wa tamasha. Aidha kwa vifaa viavyohamishika itafaa kuandaa utaratibu wa kuvipata na kuvifikisha sehemu ya tamasha.

5.3. **Fursa**

(a) Kuna watumishi wa kutosha, wenye uwezo na ari kubwa katika asasi za Serikali za kitaifa kama vile Idara ya Maendeleo ya Utamaduni, BASATA na BAKITA. Aidha uwezo wa kuhimili ongezeko la kazi litakaloletwa na Tamasha la Utamaduni la Taifa upo. Wanao uzoefu wa kuendesha matamasha walioupata enzi za Mpango Maalum wa Ukuzaji Sanaa na Lugha pamoja na kuhusika kwao katika uendeshaji wa matamasha madogo yaliyopo sasa. Ari miongoni mwa Maafisautamaduni wa Wilaya na Miji kwa tamasha hili kuanzishwa ni kubwa.

(b) Maamuzi ya kisera ya Serikali na Chama Tawala yanaounga mkono kuwepo kwa tamasha hili yanahitaji kutekelezwa.

(c) Ingawa kuna tatizo la msingi la miundombinu ya kudumu, kumekuwepo na utaratibu wa kutengeneza miundombinu ya muda kwa kutumia vifaa mbalimbali kama vile mahema. Miji mingi mikubwa inao wafanyabiashara

wanaokodisha mahema na wenye utaalamu wa kujenga miundombinu ya muda. Pia katika miji mikubwa kuna kumbi ambazo huweza kukodishwa kwa matumizi mbalimbali ya muda mfupi. Katika Shule za Sekondari na Vyuo vya Ualimu zipo kumbi ambazo zinaweza kutumika kwa shughuli za umma, hasa asasi hizi zinapokuwa zimefungwa.

(d) Wapo wataalamu wa kutosha hadi ngazi ya wilaya ambao wanaweza kutumiwa katika shughuli mbalimbali za maandalizi na uendeshaji wa tamasha. Suala la msingi ni tamasha kuwa la wadau badala ya vyombo vya serikali pekee.

(e) Udhamini wa Makampuni na asasi za biashara binafsi una uwezekano wa kukubali kuingia katika masuala ya utamaduni kwa kiwango kikubwa zaidi.

5.4. Matishio

(a) Muda wa kufanya Tamasha la Utamaduni wa Taifa ungefaa kuwa mmoja kwa miaka yote. Lakini kulingana na matukio mengine, italazimu kila mwaka kuchagua tarehe maalumu. Kimsingi miezi ya kiangazi ndiyo inayofaa, yaani Julai hadi Novemba. Lakini ni lini hasa itategemea mahali matukio kama vile Mbio za Mwenge au Mfungo wa Ramadhani na matamasha mengine kama vile ZIFF, Utamaduni wa Mzazibari, Tamasha la Bagamoyo na Tamasha la TUSEME.

(b) Ukosefu wa fedha, ikiwa pamoja na udhamini, ni tishio kubwa. Ingawa inawezekana kwa baadhi ya wadau kuwa na pesa za kushiriki, washiriki wengine wazuri watashindwa kushiriki kutokana na kukosa uwezo wa kifedha.

(c) Baadhi ya Mikoa watashindwa kabisa kuwa wenyeji wa tamasha la taifa kutokana na:

(i) Kutokuwa na miundombinu ya kudumu au uwezo wa kuandaa miundombinu ya muda.

(ii) Uongozi wa Mkoa kutokuwa na mwamko na ari ya masuala ya utamaduni.

(d) Hali iliyopo hapa nchini ya ulimbukeni wa kuthamini utamaduni wa nje inaweza kupunguza msisimko na kishindo kinachotarajiwa au hata kuibua vikundi vya wapinzani wa utamaduni wetu kulisemea vibaya tamasha hili.

(e) Kishindo cha tamasha kutokana na uzuri wa mambo yanayoonyeshwa au shughuli zinazofanyika. Uteuzi mbaya unaweza kutokea ikiwa utaratibu mzuri wa shughuli hii haukuandaliwa. Anuai ni muhimu. Lakini bila uangalifu, tunaweza kukuta, kwa mfano, mikoa 10 imeleta ngoma ya Sindimba.

(f) Kuwepo kwa matamasha mengine kunaweza kupunguza ari na mvuto wa Tamasha la Utamaduni wa Taifa. Pamoja na kwamba matamasha yaliyopo ni ya sehemu fulani tu ya nchi, fani maalumu au vikundi maalumu vya washiriki, inawezekana kabisa matamasha hayo yakaathiri vibaya Tamasha la Utamaduni wa Taifa, hasa kwa sehemu zenye matamasha hayo, vikundi vinavyohusika nayo au vikundi Maalum vya washiriki, au fani zenye matamasha yake maalumu.

6.0. Mambo Muhimu ya Kuzingatiwa

6.1. Dira, Dhamira na Madhumuni

Ili tamasha liweze kuwa na maana, ni muhimu kuwa na dira, dhamira na madhumuni yatakayokuwa wazi, kueleweka na kukubalika na wadau wote. Haya ndiyo yatawezesha kuwa na tamasha ambalo litafanikisha malengo mahsusi ya ki-utamaduni na kitaifa. Kinyume chake itakuwa ni matumizi mabaya ya muda, fedha na nguvukazi.

6.2. Mpango Mkakati

Ni muhimu kuwa na mpango mkakati wa utekelezaji ili kuwa na hakika ya mafanikio. Mpango huu uwe wa miaka mitano na utaendelea kuhuishwa maka hadi mwaka. Aidha kila mwaka kuandaliwa mpango wa kutekelezaji (Action Plan).

6.3. Mahitaji ya Fedha

Suala la kuboresha bajeti ya Sekta ya Utamaduni katika asasi na ngazi zote zitakazohusika na tamasha hili ni la msingi sana. Hii ni pamoja na Idara za Serikali, Mashirika na Halmashauri. Utaratibu wa kugawana ugharimiaji ni muhimu kusisitizwa kwa wale wote watakaokuwa na majukumu ya kuchagua na kupeleka fani katika tamasha. Aidha inafaa kutafuta vyanzo vingine kama vile ufadhili na udhamini. Ni muhimu vile vile kufikiria utaratibu wa kuanzisha Mfuko wa Tamasha ambao utawafadhili wale wakaoshindwa kabisa kupata njia zao wenyewe za kugharamia utekelezaji wa majukumu yao.

6.4. Usimamizi katika Mikoa na Wilaya

Kutokana na shughuli za Utamaduni kuendeshwa kwa kushikizwa tu katika Idara mbalimbali za Sekretariati za Mikoa, kuna matatizo ya usimamizi na uratibu. Baadhi ya Wilaya hazina Maafisa Utamaduni au waliopo hawana uzoefu wa kutosha wa kusimamia na kuendesha matamasha. Hali hii inalazimisha kuwepo kwa maelekezo na maelezo ya kina kwa watakaohusika katika ngazi hizi.

6.5. Matangazo ya Tamasha

Ni muhimu kwa tamasha hili kujulikana kote nchini na nchi za nje. Hii itasaidia kuimarisha umuhimu na kishindo chake, ikiwa pamoja na kuvutia washiriki, watazamaji na wafanya biashara.

5. Tamasha La CHASAMATA	Chama cha Sanaa za Maonyesho Tanzania	i. Kupata kukindi bora cha Mwaka ii. Kupata wasanii bora na kuwazawadia iii. Kuteua vikundi vya kushiriki Tamasha la Sanaa la Bagamoyo ZIFF	Desemba, DSM	(a) Ngonjera (b) Tamthiliya © Majigambo (d) Hadithi Simulizi (e) Ngonjera (f) Ngonjera
6. Tamashala la Ukaguru		Kusherehekkea Utamaduni wa Jamii ya Wakaguru	Agosti. Gairo	(a) Ngoma (b) Muziki asilia
7. Siku ya Kiswahili	BAKITA	Kuenzi lugha ya Kiswahili	Februari, DSM	a.Makongamano b. Maonyehso ya Vitabu c. Utoaji tuzo kwa watu waliochangia Maendeleo ya Kiswahili d. Shughuli mbalimbali za kudhihirisha uwezo wa Kiswahili kutumiwa katika nyanja za biashara, elimu na taaluma
8. Matamasha ya SADC	SADC na nchi wenyeji	i. Kuimarisha ushirikiano miongoni mwa nchi wanachama ii. Kukuza utamaduni katika nchi za SADC kupitia tasnia za	Ni uchanguzi wa nchi mwenyeji. Tamasha kila miaka miwili Ratiba ya sasa: 2004 – Muziki Zambia	a. Ngoma b. Muziki wa Kiasili na Kisasa c. Tamthilia d. Sanaa za

		utamaduni na utalii	2006 – Mchanga-nyiko 2008 – Tamtiliia, Tanzania 2010 – Mchanga-nyiko 2012 – Sanaa za Ufundi Malawi	Ufundi e.Makongamano f. Warsha g. Mikutano
9. Matamasha ya nchi za Mashariki ya Afrika	Eastern Africa Theatre Insstitute (EATI) Wanachama kwa sasa ni Tanzania, Uganda Kenya na Ethiopia	i. Kukuza Ushirikiano Miongoni mwa wasanii wa sanaa za maonyesho ii. Kubadilishana uzoefu, stadiii na utaalamu iii. Kupanua soko na hadhira ya kazi za wasanii	Uchaguzi wa nchi Mwenyeji. Ratiba ya sasa ni: 2004 – Kenya 2006 – Tanzania 2008 – Ethiopia 2010- Uganda	a. Tamthilia b. Ngoma c. Sarakasi